14 Aprili 2009

Habari za asabuhi wote,

Kama kila mmoja wetu, ulimwenguni, nimepatikana na maradhi ya kimwili, maono na kiroho na shida za kiuchumi katika dunia. Hofu ya kiuchumi ni hali ambayo inanisumbua sana maono yangu. Nilichangisha zaidi ya $20,000.00 kwa Participate Now! katika mwaka 2008, lakini minechangisha $5,000.00 tu katika mwaka 2009 mpaka sasa ambazo zitatumiwa katika awamu ya mwisho ya mradi wa wakulima wa koani, lakini sio kulipa mishahara (kama mshahara wangu wala kulipia miradi mingine ya kuanzia). Ninajisikia hofu sana na sina moyo wa kuandika barua pepe kuomba misaada. Ninafikiria kukata tamaa kabisa na kujaribu kutafuta kazi ya kulipa ili niweza kujinunulia chakula na kujilipia kodi ya nyumba. Nina hiari, ninaweza kukata tamaa, au ninaweza kujizingatiti na kuomba msaada, au niweza kuketi kimya na kujikusanya nguvu za kimoyo na halafu kuongea na watu na kupanga jinsi gani ya kufanya. Nimepanga mpango – ninaishi kwa orodha ya "matakwa na mahitaji" kama sio kitu ambacho sihitaji basi situmii pesa kukinunua. Hiyo ni rahisi. Nimeandika orodha ya matumizi yangu ya kila siku na gharama yangu ya kila mwezi ili niweze kujua ukweli wa mambo. Nimeamua kwamba sitaliwachilia shirika langu la Participate Now! kazi ninayoifanya sasa ndiyo hasa ninatakiwa kiifanya. Ninawatia moyo watu, maishi ninawavutia watu na watu wanabadilishwa kwa ajili yangu na pia maisha yangu yanabadilishwa kwa ajili ya watu ninao kutana nao. Ninaamini kwa moyo wangu wote kwamba kama nikiweka nguvu zangu zote na kufanya bidii katika kazi yangu, mimi na wengine watafaidika. Kazi yangu ni kupiga kata ngalawa sio kuiendesha.

Ndoto yangu ni kuwa na pasa za kutosha siku moja ili niweze kujitengemea bila kuomba pesa. Ndipo nitaweza kuwatumia barua pepe kuwaelezea juu ya maisha yangu mazuri na kazi yangu hapa Zanzibar. Lakini, kwa sasa, moja za kazi zangu nikuchanga pesa, ninachukia kutengemea na kuwa mhitaji, kwa hiyo ninawaomba msaada wenu, chochote kili mwezacho kutoa kitafanya tofauti kubwa. Ninataka kuchangisha $10,000.00 haraka iwezekangayo kwa mradi wa maji wa Kendwa. Tulitegemea kwamba mwenye hoteli moja hapa angeweza kutuchangia, lakini haitawezekana kwa sasa. Kitu cha kuvutia juu ya kuwa na shirika langu ni kwamba nina uweao wa kuchanga pesa na kutumia mchango huo katika mradi haraka iwezekanavyo, kutekeleza kwa hapo kwa hapo!! Sitakata tamaa kwa sababu sioni njia ingine. Sisi sote hatutakata tamaa, tafuta chochote uaminicho na usikiachilia.

"Kuwa tajiri nikuwa na cha kutosha kuweza kugawana na wingine."

Suleiman Said Mohammed

Tafadhali tuma hundi ya pesa katika anuani ya CT au kama unaishi Zanzibar unaweza kunitafuta mimi au tuma hundi ya pesa katika anuani ya Zanzibar, tuna akiba ya benki katika Zanzibar tunachukua USD au Tsh au tutembelee katika mtandao wetu wa Participate Now! ili kutuoa msaada wako kupitia PayPal.

Participate Now! Participate Now!

424 Riverside Drive
Fairfield, CT 06824 USA

P O Box 3311
Zanzibar Tanzania

Kama mnavyojua, lengo langu ni kusaidia kubadilisha kazi ya maendeleo ya kimataifa ili kuweza kafaulu na kujimudu. Mashirika makubwa ya misaada wanataka kuwafikia watu wengi kama iwezekanavyo, jambo hili ni gumu sana na lina utata kufanya kwa eneo kubwa. Unaweza kupataji mahitaji ya kweli ya watu maskini, au watu wanaohitaji ushauri na mwongozo? Hili ni swali ninaulizwa na watu wengi ninaokukuna nao, wanaofanya kazi na mashirika makubwa ya misaada. Kile ninacho ni ujuzi ambao ninajifunza – nimeishi Zanzibar zaidi ya miaka minne na nimepanga kuishi zaidi hapa. Nimetekeleza miradi midogo midogo ya kwanza ili kujifunza kutoka kwa wenyeji mahitaji yao na jinsi yakupambana na mahitaji haya kwa njia ya kufaa. Mimi sio mtaalamu, nilikuwa na biashara ndogo ya kushauri kwa miaka mingi na nilijifunza kwanza juu ya maendeleo ya kimataifa nilipotembelea Cairo hadi Capetown katika mwaka 1974. Nilihudhuria chuo kikuu cha Tufts kama mwanafunzi aliye mtu mzima na nikafuzu mwaka 2004 na shahada ya sayansi ya siasa. Nilijifunza mengi sana juu ya nchi ambazo nilizozitembelea mbeleni, nilijifunza jinsi ya kuuliza maswali na kupeleleza. Haya ndiyo ambayo nimekuwa nikifanya tangu kufika Zanzibar. Nimeambiwe kwamba sitaweza kubadilisha mwongozo wa viwanda vya maendeleo, ni kubwa sana na iliimarishwa kwa muda mrefu sana. Je! Inaamisha kwamba nisijaribu! Kuna watu wengi wenye nia njema ambao wanafanya vitu vingi mbalimbali katika nchi zinazoendelea, sauti zao nilazima zisikilizwe – tunahitaji mawasiliano kutiririka kati ya kila kikundi. Kile ninachoweza kufanya ni kujifunza kutoka kazi yangu na ujuzi wangu – ninawashirikisha watu wote na kila mtu nikitumaini kwamba wengi watakuwa na mvutio na, kuweza kuuliza maswali na kujifunza jinsi bora ya kuwasaidia watu ambao wanamahitaji zaidi – kokote waliko ulimwenguni.

Mradi wa Kendwa – Aprili 2009

Nimemaliza kuubadilisha mtandao wangu na ninaupenda. Mimi sio mtaalamu wa kutengeneza mtandao lakini nilitaka kuwa na mtandao ambao unapendeza kwa watu ambao watautembelea. Kama nyumbani kwangu. Kuna mkeka wa kukukaribisha katika mtandao na katika nyumba yangu katika Zanzibar kama ukitembelea kisiwa hiki maridhawa katika pwani ya Afrika Mashariki. Nimeongeza ukurasa wa “Miradi” pamoja na taarifa na makadirio ya fedha ya miradi yetu mitatu midogo. Madhumuni ya maji ya Kendwa ni mafupi na makadirio ya mradi wa maji wa Kendwa ni rahisi na wazi. Nimeongeza mbinu zetu ambazo ndizo jinsi tunavyozingatia kila mradi. Makadirio yanayohitajika kwa mradi wa maji ni $6,800.00. Ninatumaini kuchangisha zaidi ili kuwa na washa ya kupanga kushirikiana na wana vijiji ili kujifunza zaidi juu ya mahitaji yao, matumaini yao na ndoto zao.

Kutafuta Maji

Mambo haya yote ni kuhusu maji – na jinsi ya kuyafikia. Kijiji cha Kendwa kiko karibu na bahari ambako kuna hoteli kadhaa. Mabomba ya maji ya mahoteli haya yanapitia katikati ya kijiji hiki – kijiji hiki kinatumia visima vitatu tu. Kuna takribana watu wazima 800 na watoto 300 katika kijiji cha Kendwa ambapo kuna vijiji vidogo vidogo vinne. Wanawake inawabidi kuteka maji ambayo yako katika visima vya urefu wa mita 50 kisha kubeba majumbani kwao mara mbili kwa siku. Hawa wana kijiji wanahitaji heshema na utu – ili sauti zao kusikika. Wiki iliyopita walituomba msamaha Suleiman na mimi kwa kuwa “mburimateri” ambayo maana yake ni watu wasiojua kitu, bila elimu. Walisema kwamba tulikuja ili kuwasaidia kuelewa kwamba ni muhimu kukaa na kuzungumza kupanga na kuanzisha. Walitushukuru kwa kutumia wakati wetu nao ili kuwasaidia kuamua mpango gani ni bora kwao kuwezesha kupata maji. Wana haki kuwa na sauti ili kuweza kujua mahitaji yao ni gani na jinsi yakuyatatua. Mradi huu ambao tunafanya unalenga kupata mifiriji mitatu kwa vijiji vinne. Katika safari yangu ya kwanza waliniambia kwamba watoto watafurahi sana kama watafungua mifiriji ili kupata maji – ninatumaini nitawatumia picha za watoto wakicheza na mifiriji ya maji wiki chache zijazo.

Kushirikiana na Ramani

Participate Now! imejitoa kushirikiana – hiyo ndiyo msingi wa kazi yetu. Sisi husikiliza na hujifunza, huunda na kupanga, hushiriki na huandika na hushirikiana. Suleiman, mimi na wengine tumekuwa tukikutana na wana vijiji tangu Oktoba tukiwasikiliza na kujifunza juu ya shida za maji. Tulikutana katika chumba kando ya mskiti na karibu na madrassa ambapo watoto hunakili Koran kwa umaridadi sana. Ramani iliopo kushoto ilichorwa mara yakwanza tulipokutana na wana vijiji ili kujua hali halisi ilivyo. Ramani ya pili ili chorwa na wana vijiji ikionyesha (katika rangi nyekundu) pahali ambapo visima vipo, pahali ambapo bomba kuu la maji lipo na pahali wanapotaka kuwa na mifirji. Tumekuwa

wazi sana na kuhakikisha kwamba kila mtu amewakilishwa katika njia ya kupanga. Tumekutana na mafundi, masheha na watu mbalimbali wa serekali ya mtaa na Wizara ya Maji, ilikupata usaidizi wowote ule tuliohitaji – hatuna afisi wala gari. Tumejitolea wakati wetu, tumetumia daladala pamoja na tumeuliza kupunguziwa bei, tumetumia komputa zetu wenyewe na kuchapisha madhumuni haya.

Watoto Watakao Faidika

Je! Nani hufaidika zaidi kutokana na miradi hii? Wana vijiji na watoto wao!!!! Tumefanya kazi bega kwa bega pamoja na wana vijiji hawa ili kuwasaidia kubuni mipango ya "biashara" au "maarifa" jinsi ya kuweza kupata maji kijijini kwao kwa njia ya kudumu na heshima – wakifanya kazi na mazingira, jamii na wafanya kazi wa serekali ya mitaa. Tunatumaini kuchangisha $10,000.00 ili miezi michache ijayo tunaweza kuwa na washa ya kupanga kushirikiana kwa wiki moja. Tunataka kuchukua muda ili kusikiliza kwa makini mambo wanayoyasema. Tunataka watu kweli kuwa na sauti zao – kuwasaidia kuweza kuona kwa hakika mahitaji yao na baadaye kuwasaidia kupanga mipango ambayo yataambatana na mahitaji yao. Sio mimi wala mtu yeyote mwingine anaweza kuamua ukuu wa mambo ya wana vijiji. Mimi kila mara huuliza swali "unawezaje kudhihirisha kufaulu?" Sitajua wana kijiji wa Kendwa wanavyodhihirisha kufaulu mpaka nitakapowauliza na halafu nichukue wakati kuwasikiliza kwa makini wanachosema.

Kijiji cha Kendwa kimekuwako toka karne na karne – zamani sana hata kabla ya mahoteli kuwako. Patakuwako hata baada ya mahoteli kubadilisha wamiliki au kuondoka. Tunatumaini kupanga pamoja na mahoteli kuwa na mchango wa pamoja siku za usoni ambao utasaidia sana – baada ya wana kijiji kuwa na mpango maalum wazi na kujua majitaji yao ya kwanza. Tuwasaidia hawa watu kuwa na sauti yao – tafadhali toa mchango ili tuweze kuwaletea maji. Wanaume watachimba mitaro wenyewe na kujenga nguzo za kila mfireji. Tunaweza kuwa na maji baada ya siku 2 au 3 tukiwa na pesa za kutosha. Tafadhali tusaidie kukamilisha jambo hili.

Kama hutaki kupata barua pepe kama hii kwa siku za usoni – tafadhali niandikie mimi na nitaweze kukutoa katika orodha hii. Ninaelewa kabisa kwamba ni vigumu kusoma barua ndefu sana.

Tutembelee katika mtandao wetu: http://www.participatenowfoundation.org ili ujifunzi juu ya shirika letu. Lengo letu ni kufanya miradi midogo midogo ambayo inamatokeo ya kudumu. Tunashukuru kwa msaada wowote ule ambao unaweza kutupa.

Participate Now!
424 Riverside Drive
Fairfield, CT 06824 USA

Participate Now!
P O Box 3311
Zanzibar Tanzania

Asante sana kwa kusome barua hii.

Kathryn
Director
Participate Now!
http://www.participatenowfoundation.org
http://www.kathrynsutton.com